JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
MFUKO WA MISITU TANZANIA

Kwa Kudumisha Ugharimiaji wa Usimamizi wa Misitu

# MAFANIKIO YA MFUKO WA MISITU TANZANIA



2022

# 1. UTANGULIZI

Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) ni Mfuko wa Serikali ulioanzishwa chini ya Sheria ya Misitu Sura 323 kwa lengo la kuwa chanzo cha uhakika na endelevu cha fedha kwa ajili ya kuwezesha na kugharamia uhifadhi, usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali misitu nchini. Mfuko upo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii na unasimamiwa na Bodi ya Wadhamini ambapo shughuli za kila siku zinafanywa na Sekretarieti ya Mfuko. Mfuko wa Misitu Tanzania ulizinduliwa kupitia Waraka wa Hazina Na. 4 wa mwaka 2009/2010 na ulianza rasmi utekelezaji wa majukumu yake Julai 2011.

## 1.1 Dira, Dhamira na Misingi ya Utendaji

**Dira** ya Mfuko wa Misitu Tanzania ni kuwa Taasisi inayoongoza kuwa na chanzo endelevu cha fedha kwa ajili ya kuwezesha na kugharamia uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za misitu.

**Dhamira** ya Mfuko wa Misitu Tanzania ni kuhakikisha upatikanaji wa fedha na kuwezesha na kugharamia ulinzi, uhifadhi, usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali misitu Tanzania.

Katika utendaji wake, Mfuko wa Misitu Tanzania unaongozwa na misingi mikuu mitano (5) ambayo ni:

i) **Uwazi:** Tunafanya kazi kwa uwazi na usahihi katika kutekeleza majukumu;

ii) **Uwajibikaji:** katika kutoa huduma kwa weledi na ufanisi na kubeba dhamana ya maamuzi ya kiutendaji;

iii) **Uadilifu:** kwa kuzingatia maadili na uaminifu katika kutoa huduma;

iv) **Ushirikiano katika kufanya kazi:** kwa kufanya kazi kwa pamoja na kwa kuzingatia weledi na ubora; na

v) **Haki na Usawa:** Huduma inatolewa kwa kuzingatia haki na usawa.

## 1.2 Malengo na Majukumu ya Mfuko wa Misitu Tanzania

Mfuko wa Misitu Tanzania una malengo na majukumu saba (7) yaliyoainishwa katika kifungu cha 80 cha Sheria ya Misitu Sura 323 kama ifuatavyo:

(i) Kuwezesha uhamasishaji jamii kupitia elimu na mafunzo kuhusu umuhimu wa uhifadhi, usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali misitu;

(ii) Kuwezesha na kugharamia uhifadhi, usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali misitu kupitia utoaji ruzuku kwa vikundi na wadau wengine wanaojihusisha na uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu;

(iii) Kukuza, kuendeleza na kugharamia utafiti kwa lengo la kuboresha na kuimarisha uhifadhi, usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali misitu;

(iv) Kusaidia na kuiwezesha Tanzania kunufaika na mipango na misaada ya Kitaifa na Kimataifa kwa engo la kuboresha na kuimarisha uhifadhi, usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali misitu;

(v) Kusaidia na kuwezesha vikundi na watu binafsi kushiriki katika mijadala na midahalo ya masuala ya misitu na kuandaa tathmini za kimazingira kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 18 cha Sheria ya Misitu Sura 323;


(vi) Kusaidia na kuwezesha vikundi na watu binafsi ili wafuate Sheria ya Misitu, Kanuni na miongozo mbalimbali; na

(vii) Kugharamia shughuli nyingine zinazoendana na majukumu ya Mfuko wa Misitu Tanzania na shughuli zinazohusiana na madhumuni ya Sheria ya Misitu Sura 323.

## 2. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 10 KUANZIA MWAKA 2011/2012 HADI MWAKA 2021/2022

Katika kipindi cha miaka kumi (10) ya utekelezaji wa majukumu ya kugharamia uhifadhi, usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali misitu, Mfuko wa Misitu Tanzania umepata mafanikio yafuatayo:

**2.1** Kutoa ruzuku kwa miradi **738** yenye mchango katika ulinzi, uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu. Miradi iliyopatiwa ruzuku na Mfuko inatekelezwa katika wilaya 115 (Kielelezo Na. 2). Vilevile, idadi ya mikoa yenye miradi iliyopatiwa ruzuku imeongezeka kutoka mikoa 7 mwaka 2011/2012 hadi kufikia mikoa 26 mwezi Juni 2022.




**Kielelezo Na. 1:** Miradi iliyopatiwa ruzuku na Mfuko kuanzia mwaka 2011/2012 hadi tarehe 30 Juni, 2022.

**2.2** Kuchangia azma ya uchumi wa viwanda kwa kugharamia ujenzi na ununuzi wa mitambo ya viwanda 5 vya kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki katika mikoa ya Tabora (Wilaya za Sikonge na Nzega), Geita (Wilaya ya Bukombe), Kigoma (Wilaya ya Kibondo) na Katavi (Wilaya ya Mlele). Kielelezo Na. 2 kinaonesha mitambo ya kiwanda cha kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki iliyofungwa kwenye kiwanda cha mazao ya nyuki.



**Kielelezo Na. 2:** Mitambo ya kiwanda cha kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki

**2.3** Kufanikisha upatikanaji wa malighafi (miti) kwa ajili ya viwanda vya mbao na nguzo za umeme na simu, na matumizi mengine. Mfuko umegharamia upandaji miti katika eneo

lenye ukubwa wa hekta 12,760 ikiwemo mashamba 13 ya Taasisi za Serikali (Kielelezo Na. 3). Aidha, upatikanaji wa malighafi (miti) kwa ajili ya viwanda vya mbao na nguzo za umeme na simu, na matumizi mengine kunachangia pato la Taifa kwa kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kuagiza samani na nguzo za umeme kutoka nje ya nchi, na kuongeza ajira.



**Kielelezo Na. 3:** Shamba la miti la Gereza la Isupilo lililopatiwa ruzuku ya TaFF

**2.4** Kufanikisha uboreshaji wa maabara ya mbegu za miti katika Kituo cha uzalishaji wa mbegu za miti kilichopo mjini Morogoro kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji endelevu wa mbegu bora za miti. Mfuko umegharamia upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya maabara kwa lengo la kuhifadhi na kutunza mbegu za miti kwa muda mrefu bila kuharibika (Kielelezo Na. 4). Uwepo wa maabara ya kisasa katika Kituo cha uzalishaji wa mbegu za miti kunapunguza matumizi ya fedha za kigeni za kuagiza mbegu bora za miti kutoka nje ya nchi na kunawezesha upandaji wa miti kibiashara kwa maendeleo endelevu ya misitu.




**Kielelezo Na. 4:** Vifaa vya kisasa vya maabara ya mbegu za miti vilivyonunuliwa kwa kutumia ruzuku ya Mfuko

# RAMANI INAYOONESHA MIRADI ILIYOPATIWA RUZUKU YA MFUKO WA MISITU TANZANIA NA MGAWANYO WAKE KIMKOA

**Idadi ya Miradi: 24**
Ruzuku ndogo: 11
Ruzuku ya kati: 4
Ruzuku kubwa: 7
Ruzuku maalum: 2


**Idadi ya Miradi: 13**
Ruzuku ndogo: 7
Ruzuku ya kati: 5
Ruzuku kubwa: 1

**Idadi ya Miradi: 16**
Ruzuku ndogo: 13
Ruzuku ya kati: 1
Ruzuku kubwa: 2

**Idadi ya Miradi: 2**
Ruzuku ndogo: 0
Ruzuku ya kati : 1
Ruzuku kubwa: 1
Ruzuku maalum: 0

**Idadi ya Miradi: 20**
Ruzuku ndogo: 14
Ruzuku ya kati: 3
Ruzuku kubwa: 3

**Idadi ya Miradi: 12**
Ruzuku ndogo: 6
Ruzuku ya kati: 3
Ruzuku kubwa: 3





**Idadi ya Miradi: 14**
Ruzuku ndogo: 10
Ruzuku ya kati: 1
Ruzuku kubwa: 2
Ruzuku maalum: 2

**Idadi ya Miradi: 24**
Ruzuku ndogo: 16
Ruzuku ya kati: 5
Ruzuku kubwa: 3

**Idadi ya Miradi: 28**
Ruzuku ndogo: 17
Ruzuku ya kati: 4
Ruzuku kubwa: 2
Ruzuku maalum: 5

**Idadi ya Miradi: 16**
Ruzuku ndogo: 12
Ruzuku ya kati: 4
Ruzuku kubwa: 0

**Idadi ya Miradi: 24**
Ruzuku ndogo: 8
Ruzuku ya kati: 9
Ruzuku kubwa: 6
Ruzuku maalum: 1




Ruzuku maalum: 1

**Idadi ya Miradi: 7**
Ruzuku ndogo: 3
Ruzuku kati: 2
Ruzuku kubwa: 2

**Idadi ya Miradi: 9**
Ruzuku ndogo: 6
Ruzuku ya kati: 2
Ruzuku kubwa: 1

**Idadi ya Miradi: 81**
Ruzuku ndogo: 60
Ruzuku ya kati: 16
Ruzuku kubwa: 5
Ruzuku maalum: 0

**Idadi ya Miradi: 34**
Ruzuku ndogo: 26
Ruzuku ya kati: 1
Ruzuku kubwa: 6
Ruzuku maalum: 1

**Idadi ya Miradi: 46**
Ruzuku ndogo: 33
Ruzuku ya kati: 7
Ruzuku kubwa: 3
Ruzuku maalum: 3

**Idadi ya Miradi: 42**
Ruzuku ndogo: 26
Ruzuku ya kati: 5
Ruzuku kubwa: 7
Ruzuku maalum: 4

**Idadi ya Miradi: 26**
Ruzuku ndogo: 4
Ruzuku ya kati: 9
Ruzuku kubwa: 5
Ruzuku maalum: 8

**Idadi ya Miradi: 38**
Ruzuku ndogo: 19
Ruzuku ya kati: 5
Ruzuku kubwa: 11
Ruzuku maalum: 6

**Idadi ya Miradi: 40**
Ruzuku ndogo: 17
Ruzuku ya kati: 11
Ruzuku kubwa: 12

**Idadi ya Miradi: 20**
Ruzuku ndogo: 11
Ruzuku ya kati: 3
Ruzuku kubwa: 2
Ruzuku maalum: 4

**Idadi ya Miradi: 31**
Ruzuku ndogo: 1
Ruzuku ya kati: 2
Ruzuku kubwa: 24
Ruzuku maalum: 4

**Idadi ya Miradi: 4**
Ruzuku kubwa: 2
Ruzuku Maalum: 2

**Idadi ya Miradi: 19**
Ruzuku ndogo: 15
Ruzuku ya kati: 3
Ruzuku kubwa: 1
Ruzuku maalum: 1

**SONGWE**
**Idadi ya Miradi: 9**
Ruzuku ndogo: 3
Ruzuku ya kati: 1
Ruzuku kubwa: 3
Ruzuku maalum: 2

**Idadi ya Miradi: 5**
Ruzuku ndogo: 2
Ruzuku ya kati: 0
Ruzuku kubwa: 2
Ruzuku maalum: 1

**2.5** Kuchangia uboreshaji wa maisha ya jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu kupitia ufugaji nyuki kwa lengo la kuongeza kipato na kupunguza uharibifu wa misitu. Mfuko umegharamia mafunzo ya ufugaji bora wa nyuki na utengenezaji mizinga bora ya nyuki, pamoja na kutoa jumla ya mizinga 29,063 ya nyuki kwa vikundi 612 vya ufugaji nyuki (Kielelezo Na. 5).



**Kielelezo Na. 5:** Mizinga ya nyuki iliyotengenezwa kwa kutumia ruzuku ya Mfuko

Aidha, Mfuko umewezesha vifaa vya kuboresha ufugaji nyuki (seti za mavazi ya kinga, chujio za asali, bomba za kufukiza moshi, mashine ndogo za kukamua asali na vifungashio) kwa vikundi 612 vya ufugaji nyuki. Ufugaji nyuki unachangia ajira mbadala ambayo hupunguza uharibifu wa misitu na kuongeza mchango wa sekta ya maliasili katika pato la Taifa. Aidha, ufugaji nyuki unachangia uchavushaji wa mazao ya chakula na hivyo kuchangia upatikanaji wa chakula.

**2.6** Kufanikisha upatikanaji wa vitendea kazi na vifaa vya kisasa vya utafiti misitu. Mfuko umewezesha Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) kupata magari, mashine ya kupima ubora wa mbao (Kielelezo Na. 6), vifaa na vitendea kazi vingine, na miongozo ya kusimamia na kuratibu utafiti wa misitu na nyuki.




**Kielelezo Na. 6:** Mashine ya kupima ubora wa mbao iliyonunuliwa kwa kutumia ruzuku ya Mfuko.

**2.7** Kuanzisha programu maalum ya kushirikisha wanafunzi katika uzalishaji wa miche ya miti na upandaji miti shuleni na maneo jirani.

Mfuko umebuni na kugharamia miradi ya uanzishwaji wa vitalu vya miti na upandaji miti katika shule 123 za msingi na sekondari zilizopo katika wilaya 31 za mikoa 8 yenye maeneo kame. Mikoa hiyo ni Dodoma, Singida, Simiyu, Shinyanga, Kagera, Manyara, Arusha na Kilimanjaro.



**2.8** Kupata Hati Safi kwa miaka 10 ya utendaji wake na kupewa Tuzo ya Taifa ya Utendaji Bora.

Mfuko wa Misitu Tanzania umepata Hati safi ya ukaguzi wa hesabu kwa miaka 10 kuanzia 2011/2012 hadi 2021/2022. Aidha, Mfuko umepewa Tuzo ya Taifa ya utendaji bora wa Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa kuwa mshindi wa pili kati ya Mifuko 21 iliyoshindanishwa.

